

MAKUBALIANO YA KUKABIDHI MTOTO KWA MTU MCHANGA NA ONDOLEO LA DHIMA

Tafadhali soma kwa umakini kabla ya kuweka sahihi.

Ninaelewa na kukubali kwamba, kama ilivyoainishwa katika fomu hii ya Idhinisho la Uchukuaji, nimempa ruhusa mtu mwenye umri wa **kati ya miaka 14 na 18** ("Mtu Mchanga") kuchukua mtoto /watoto wafuatao, ambao mimi ni mzazi/mlezi kwao, kutoka Rocketship.

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa: _____

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa: _____

*(ongeza nyongeza ya watoto,
ikihitajika)*

Ninaelewa na kukubali kwamba Mtu (Watu) Mchanga PEKEE aliyeorodheshwa kwenye Fomu yangu ya Idhinisho la Uchukuaji, ndiye atakayeruhusiwa kuchukua mtoto/watoto walioorodheshwa hapo juu.

Ninaelewa na kukubali kwamba Watu Wachanga wote watahitajika kuwasilisha kadi rasmi ya ruhusa ya "Idhinisho la kuachiliwa kwa mtu mchanga" ya Rocketship kabla ya Rocketship kumpatia mtoto yoyote kwa Mtu Mchanga huyo.

Ninaelewa na kukubali kwamba Rocketship haitowajibika kufuatilia tabia za mtu mchanga yeyote, ndani au nje ya eneo la Rocketship.

Ninaelewa na kukubali kwamba, Rocketship ina wajibu wa kulinda afya na usalama wa wanafunzi wote wa Rocketship wakati wanafunzi wakiwa ndani ya eneo la Rocketship. Ikiwa Rocketship itakuwa na sababu yoyote ya kushuku kuwa, afya ama usalama wa mwanafunzi yoyote wa Rocketship utawekwa hatarini kwa kumuachilia mwanafunzi huyo kwa mtu mchanga, hata pale ijapo mtu mchanga huyo amepewa ruhusa ya kumchukua mwanafunzi huyo, Rocketship ina haki ya kumshikilia mtoto huyo kwenye eneo la chuo na kuwasiliana na mzazi/mlezi ama mtu mwingine sahihi wa dharura.

Ninaelewa na kukubali kuridhia hatari zote na zozote zinazohusiana na kumkabidhi mtoto/wangu kwa Mtu Mchanga zinazoweza kujitokeza baada ya mwanafunzi kuondoka eneo la Rocketship akiwa chini ya usimamizi wa mtu huyo mchanga. Daima naondoa, naachilia, na kuitoa Elimu ya Rocketship pamoja na wakala, wafanyakazi, wakurugenzi, maofisa, na wadhamini wake kutoka kwenye dhima yoyote na zote za madhara au jeraha lolote lililosababishwa moja kwa moja na kukabidhiwa mtoto/watoto wangu kwa mtu mchanga.

Ichapishwe na Mzazi/Mlezi

Jina _____

Anuani _____

Namba za Simu _____

SAHIHI _____ Tarehe: _____